HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA

SHULE YA SEKONDARI SHIBOLYA

S. L. P 2125

MBEYA

Kumb. Na. MDC/SHSS/JI/FI 2021 **Tarehe.....**

Kwa mwanafunzi _____

S. L. P _____

MBEYA.

YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SHIBOLYA KIDATO CHA KWANZA (JOINING INSTRUCTIONS) MWAKA 2021

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Shibolya mwaka 2021. Unatakiwa ufike shuleni SHIBOLYA Jumatatu tarehe 11/1/2021 saa mbili asubuhi na mzazi wako ukiwa na vifaa pamoja na mahitaji yote kama ilivyoainishwa ili uweze kuanza masomo yako jumatatu tarehe 11/1/2021 bila usumbufu.

Jumuiya ya Shibolya inapenda kujifunza kutoka kwako kama wewe utakavyojifunza kutoka kwetu. Unapaswa kutumia muda wako katika mazingira ya shule hii kuendeleza kipaji chako ulichojaliwa na MUNGU katika TAALUMA na MICHEZO kwa ajili ya faida yako na Taifa kwa ujumla. Usiporipoti baada ya wiki mbili kuanzia tarehe ya kujiunga na shule tarehe 11/12021 nafasi yako itachukuliwa na mwanafunzi mwingine.

Pamoja na barua hii naambatanisha yafuatayo:-

1. Sheria za shule
2. Orodha ya mahitaji ya shule
3. Fomu ya kupima afya (Medical examination form)
4. Fomu ya ahadi ya mwanafunzi na mzazi mlezi
5. Hati ya kukubali sheria za shule

Unatakiwa kuleta kivuli (photocopy) cha cheti cha kuzaliwa unapokuja kujisajili kama mwanafunzi wa shule ya sekondari Shibolya.

Nakushauri uyasome maelekezo / maagizo kwa makini na utulivu ili uyaelewe na kisha utekeleze ili uondokane na usumbufu au matatizo yatakayoweza kujitokeza kwa kutotimiza maagizo ipasavyo.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI SHIBOLYA; ELIMU NI HAZINA

.....

NGONDE G. E

MKUU WA SHULE

1. MAELEZO

Soma kwa makini ili uzielewe sheria na taratibu za shule na kisha ujaze hali ya kuridhia sheria hizo. Uweke saini kwenye fomu na urejeshe shuleni.

2. KUFIKA SHULENI

Mwanafunzi unatakiwa kufika shuleni siku za masomo saa moja asubuhi, tayari kwa shughuri zote za shule. Ratiba ya shule huanza na usafi wa mazingira kabla ya kuingia darasani kwa masomo yaliyopangwa.

3. SARE SHULENI

a) Soksi jozi mbili nyeupe kwa wasichana na wavulana
b) Suruali 1 rangi kijani mgomba na 1 bluu bahari. Shati 2 rangi nyeupe tetron mikono mifupi na vest nyeupe 2
c) Wasichana sketi 1 kijani mgomba na 1 bluu bahari. Shati 2 rangi nyeupe mikono mifupi sidiria nyeupe 2 au shumizi 2
d) Sampuli ya vitambaa imefungiwa ndani ya fomu hizi.
e) Sweta 1 rangi ya kijani mgomba na 1 bluu bahari.

4. NGUO ZA MICHEZO

a. Raba jozi moja kwa wavulana na wasichana
b. Bukta 2 na T- shirt (wavulana)
c. Bkta na sketi ya michezo na T- shirt(wasichana)

ANGALIZO

5. ***Sare ya shule inatakiwa kushonwa kiheshima kwa wasichana sketi ziwe za kufunika kiwiko cha mguu na marinda yasiyopungua kumi na sita. Ni marufuku kuvaa miregezo na suruali iwe na malinda mawili na isiwe ya kubana yenye "turn up"***
6. TABIA NA MWENENDO

i. Ipende shule yako, walimu na wanafunzi wenzako. Ishi kwa amani na upendo hapa shuleni, ugomvi wa aina yoyote hapa shuleni ni marufukufu. Kauli zako wakati wote zioneshe busara na kudhihirisha uzalendo wako.
ii. Mali ya shule pamoja na yako binafsi ni lazima zitunzwe vyema. Kufanya kitendo chochote kinachoweza kuharibu mali ya shule au mali yako ni kosa kubwa. Kutokana na uzito wa kosa unaweza kufukuzwa shule kwa uharibifu wa mali.
iii. Nidhamu inahitajika darasani na nje ya darasa. Marufuku kupiga kelele darasani kwani ni usumbufu kwa wengine wenye kupenda mafanikio. Usitoke darasani bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi wa darasa mtindo wa kuzomeana hapa shuleni ni marufuku kwani si uungwana.
iv. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kusimama kwa adabu mwalimu anapoingia darasani au anapopita. Jibu swali au uliza swali ukiwa umesimama.
v. Iwe ni kawaida kwa mwanafunzi kumpkea mgeni yeyote au mwalimu mzigo hapa shuleni. Simama na salimia kwa heshima wakati mgeni au mwalimu anapopita.
vi. Ni lazima kila mwanafunzi aheshimu bendera ya Taifa na picha za viongozi wa Taifa. Kinyume chake mwanafunzi atachukuliwa hatua kali.
vii. Mwanafunzi lazima aheshimu ofisi za

- Mkuu wa shule
- Makamu mkuu wa shule
- Walimu
- Karani

viii. Ni marufuku kuingia nyumba ya mwalimu bila ruhusa ya mhusika au mkuu wa shule

ix. Mwanafunzi anapozungumza na mwalimu au mkubwa yeyote si vema tena ni marufuku kuweka mikono mifukoni au kushika kiuno au kubishana kwa daharau.

x. Pia mwanafunzi anapoitwa na mwalimu au mkubwa teyote lazima aende kwa kukimbia

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kushiriki katika aina yoyote ya ulevi, uvutaji sigara, wala kuingia kwenye majumba ya starehe / kufikia wageni (guest houses)

7. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

1. Heshimu viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii yote kwa ujumla
2. Hudhuria shughuli ndani na nje ya darasa
3. Wahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa
4. Fahamu mipaka ya shule na zingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka wakati wote wa uanafunzi katika shule hii.
5. Tunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
6. Vaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
7. Zingatia ratiba ya shule wakati wote

8. MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE

1. WIZI
2. UASHERATI
3. ULEVI WA POMBE NA MATUMIZI YA MADAWA YA KULEVYA KAMA KUVUTA BANGI
4. MAKOSA YA JINAI
5. KUPIGANA AU KUPIGA
6. KUDHARAU BENDERA YA SHULE/TAIFA
7. KUOA AU KUOLEWA
8. KUHARIBU KWA MAKUSUDI MALI YA UMMA
9. KUPATA MIMBA AU KUSABABISHA MIMBA NDANI AU NJE YA SHULE
10. KUTOA MIMBA
11. KUGOMA, KUCHOCHEA NA KUONGOZA AU KUVURUGA AMANI NA USALAMA SHULE AU WATU
12. KUKATAA ADHABU KWA MAKUSUDI
13. MWANAFUNZI KUWA NA SIMU SHULENI

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI SHIBOLYA UFUFUE VIPAJI VYAKO KITAALUMA NA KATIKA MICHEZO

ELIMU NI HAZINA

.....

NGONDE G.E

MKUU WA SHULE

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA
SHULE YA SEKONDARI SHIBOLYA

FOMU YA AHADI YA MWANAFUNZI NA MZAZI / MLEZI

A. SEHEMU YA MWANAFUNZI

a) Mimi ..... msichana/ mvulana, nakubali kuingia kidato cha ..... Katika shule ya sekondari Shibolya kama mwanafunzi wa kutwa nitafika shuleni tarehe iliyoelekezwa bila kukosa au kuchelewa.
b) Nitatii sheria zote za shule kama zinavyosomeka na nitaishi maisha mazuri ya mfano. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za kujitegemea sitakuwa mtoro shuleni, wala kuwa mwanafunzi mwenye usumbufu.

Sahihi ya mwanafunzi ..... Tarehe .....

B. SEHEMU YA MZAZI / MLEZI

1. Mimi ..... Ninakubali mtoto wangu kwa jina ..... asome katika shule ya sekondari Shibolya kuanzia kidato cha kwanza. Naamini kuwa elimu ni urithi wa mtoto na mwanga wa maisha.
2. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote anayotakiwa kuwa nayo shuleni kama ulivyoagiza kwenye barua yako nitatoa na kutekeleza kwa wakati bila usumbufu wowote.
3. Nitahakikisha kuwa nitamkanya mtoto wangu kutii kanuni na sheria za shule na nitahimizwa asiwe mtoro kwa kutoa ushirikiano kwa walimu na serikali kwa ujumla katika malezi ya mtoto
4. Ninakubali kuwa mtoto wangu amekubali kusoma katika shule ya serikali ya sekondari ya Shibolya na sitamhamisha kwenda shule nyingine pasipo sababu ya msingi
5. Anuani yangu ya kudumu ni

Sahihi ya mzazi/ mlezi ..... Tarehe .....
S. L. P .....
.....
Namba ya simu .....
Barua pepe kama unayo .....

C. KWA MATUMIZI OFISI TU

Mwanafunzi .....amepokelwa tarehe.....
anamapungufu yafuatayo

1. .....
2. .....
3. .....
4. .....
5. .....
6. .....
7. .....

SAHIHI ..... JINA .....

MWALIMU ANAYEMPOKEA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA

SHULE YA SEKONDARI SHIBOLYA

S. L. P 2125

MBEYA

Medical officer
Government hospital
P. O BOX .....
.....

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examine .....9student) as to her / his fitness for nursing further education at this school.

.....
NGONDE. G.E
MKUU WA SHULE

1. Hemoglobin .....
2. P.V. Bleeding .....
3. Blood pressure .....
4. Blood Group .....
5. Hearing .....
6. Sight .....
7. Urine for sugar both boys and girls .....
8. Pregnancy for girls only .....
9. Stool for routine examination .....
10. Asthma .....
11. Skin diseases .....
12. Epilepsy .....
13. Leprosy .....
14. Deformity .....
15. Pulmonary tuberculosis .....
16. Mental problems .....
17. V.D. (give type) .....
18. Any other serious disease not mentioned above

.....

OTHER COMMENTS .....

.....
Designation signature and official stamp